# Je, umesikia ?

* KUWA mjini Bukavu wakaaji na wapita njia hasa wadereva watishwa bado na hali ya mabarabara? Je ? Kwa kuwa tu mashimo yaendelea kuchimbua siku kwa siku isiwe tu na maji ya mvua bali pia na hilo shirika la SOZAGEC lenyi kuhusika na kutawanya mirija ya maji safi ya kunywa baada ya kuchimba mashimo hayo haliyazibi kama inavyohitajika mahali kazaa. Lakini mshangao mkubwa ni kuona kama viongozi na wakuu jimboni ambao walihaidia kutengeneza kilometri 20 ya mabarabara mjini wakikabiza kiasi fulani cha feza kwa shirika lenyi ujuzi wa kazi hawajakohoa hata ili raïa wangojee matunda mazuri ya feza zilizotolewa na Serkali kuu. Na baada ya kupiga kelele na kuziba masikio ya wanachama na wageni eti kilometri 6 zitatengenezwa upya, mjini, leo hii nenda, kuja na kajionee yaliyoko. Eti hiyo ndiyo namna bora ya kutuonya kama kazi zatumikwa kweli makwetu.

* KAMA wananchi wengi waliochukuliwa kunako shirika lenyi kuhusika na foroza (OFIDA) kama vile watumishi watoka Kinshasa ao kwao na kiongozi wa shirika hilo jimboni mwa Kivu ya zamani ?

Hum ! Watu wengi hunungunika kama sisi kwani kazi hao jamaa waendesha kweli zaweza kuendeshwa na wengine wananchi waliotuma ombi lao la kazi kwenyi «mkuu» huyo. Unyonge wa watu ni kuona kama wafanyakazi hao toka huko mbali walisafirishwa na wapangishwa, wasemavyo mjini Bukavu, na shirika ama ndugu bora tu wajue namna ya kuwinia miongoni mwa wakaaji bila kusahau kuwapaka mafuta waliowatuma.

Kumbe hiyo ndiyo namna ya kuwasaidia ndugu na kusirimusha vizuri viziwi na vipofu. Pia kupinga ubaguzi wa makabila nchini.

* KWAMBA feza zilizotolewa na Serkali kuu kwa kutengeneza upya mabarabara na vilalo kwa kusafirisha watu, mazao na mavuno ya mlimo vilayani kama vile vijijini hadi mahali vinavyohitajika zilinyongwa na wananchi wasio na zamiri njema ya kimapinduzi.

Yasemekana kuwa wengi waliotezamiwa kupewa feza hizo kama vile mashirika, jimboni mwa Kivu ya Kusini walilazimishwa kurudisha kiasi kilichoombwa na «wabwana kuu» kwa manufaa yao wenyewe. Kiasi kingine, wanena wamoja kati ya watumishi Serkalini, chatumiwa kwa nusu ya kazi hizo za mabarabara ao hapana na kingine chatiwa mfukoni mwa waliokabizwa. Ni hiyo baada ya kuitika kweli kwa maandiko wakitia sahihi na mhuri wao kwenyi vikartasi vya Serkali eti walipata feza zote zilizotolewa. Eti hiyo ndio ginsi ya kutumikia mapinduzi na kusaidia Raïs Mobutu, Baba wa Taifa, katika siasa aendesha kwa kurahisisha maisha kijamii ummani. Loo !

* KAMA wakaaji wa Uvira wanungunika kubadilishwa kwa mwenyekiti wa zamani wa mtaa huo ? Labda. Lakini yaliyo kweli ni kusikia kama kiongozi huyo alipendelea sana kusali na kutawanya neno la Mungu nyumbani mwa wakaaji ingawa hawa, wengi kati yao, mabati (majanja) na paa zilirushwa mara na mara na upepo mkali na mvua. Na toka hapo hakuna hata msaada mmoja uliweza kutolewa na Serkali kukabizi kwa walio na wanaohusikia na hali hiyo. Nenda kajionee soko kuu na shule la maelimisho la ufundi huko. Mtu ambaye atakayeyaokowa si mwengine bali kiongozi wa sasa. Kumbe huko si kiongozi Serkalini kaende bali ni pastori. Aah ?

# DAFTARI KAMILI YA WANAMEMBA WA SERKALI

Hapo majuzi Prezidenti-muundaji wa Chama cha Mapinduzi, Mareshali Mobutu, kabadili wenyekiti madarakani katika Chama-serkali. Mabadiliko kafanya Baba wa Taifa yaonya kuwa ahusika na mwenendo bora unaopaswa kuwekokatika kazi zaendeshwa kwa manufaa ya taifa toka hapo urahisi wa siasa ya uchumi, ujamii na kazalika.

Kunako ukatibu mkuu wa Chama, katibu mkuu abaki mwananchi Kithima bin Ramazani na naibu wake kwa sasa ni wananchi Mpinga Kasenda na Vunduawe Te Pemako. Katibu imara kunako Kamati kuu ya Chama ni Umba di Lutete, Singa Udjuu katajwa kama vile katibu imara na mwanamemba wa Chumba cha siasa, Sakombi Inongo kama vile katibu mtendaji kwenyi uhimizaji wa chama na jemadari Manzembe ma Ebanga wote wawili katajwa wanamemba wa Kamati kuu ya chama.

Kunako baraza la mawaziri, waziri mkuu na makamu wake wabaki Kengo wa Dondo, Nimy Mayidika Ngimbi, Mwando N'Simba na Mozagba Ngbuka.

Mawaziri wengine ni wananchi : Jemadari Singa Boyenge Mosambayi (usalama wa nchi), Ngunz a Karl-I-Bond (mashauri ya kigeni), Niwa Mobutu (uhusiano baina ya mataifa), Ngongo Kamanda (upashaji wa habari), Bofossa w'Ambea Nkoso (miradi ya serkali), Katanga Mukumadi ya Mutumba (hazina na fedha), Mananga ma Pholo (utumizi wa fedha), Takizala Luyanu (ukulima), Banguli Nsambue Mbali (uchumi), Kisanga Kabongelo (viwanda vidogo), Nzanda Bwana Kalemba (biashara na nchi za kigeni), Mushobekwa Kalimba (kazi na nguvu za umeme), Kibangula kia Makongo (kazi na ujenzi wa nchi), Sampasa Kaweta Milombe (usafiri), Jemadari Likulia Bolongo (ardhi), amirali Lomponda wa Botende (mazingira na ukingo wa maumbile), Bayona Ba Meya (Elimu ya juu na utafuti wa kisayansi), Nzege Alaziambina (masomo ya msinji na ya sekondari), Pendje Demodeto (afya), Nzungu Luntadi (makazi ya wananchi), Ngandu Kabeya (jamii) Muduka Inyanza (kazi na mategemeo ya kijamii), OkitakulaDjambokota (watumishi wa serkali), Ileo Itambala (posta), Kibassa Maliba (Michezo), Ileką Nkumu (utamaduni na utalii).

Majina yafuatayo ni ya makatibu wa serkali : Mavua Mudimba (ulinzi), Babia Zongbi Malobia (askari jeshi wa zamani), Yende Buku (usalama), Muyabo Nkulu (sheria), Sabi N g a m p o u b Mubiem (haki za raïa), Ikolo Bolelama na Ibula Mwana Katakanga (mashauri ya ndani), Buketi Bukayi (mashauri ya kigeni), Malu wa Koni (uhusiano wa kimataifa), Ilunga Ilukamba (miradi), Kwini N'Sel (hazina), Bombito Botomba (matumizi ya fedha), Mubenga Mukendi (ukulima), Kitenge Tabu Yemba (maendeleo ya vijiji), Kiro Kimathe Ndato (maadini na nguvu za umeme), Bingoto Mangoto (kazi na ujenzi wa inchi), Mulamba Musambay (usafiri), Diur Katond (elimu ya juu na utafiti wa kisayansi), Nzali Lopembe (masomo ya msinji na sekondari), Lobo Kanza-Kanza (mazingira na ukingo wa maumbile), Sendwe Kasongo Ilunga (watumishi wa serkali).

Bisimwa L.B.
na Lubunga B.


**ANGALISHO !**

Zaidi ya watu
10.000 wanagonjwa
SIDA
TUJIKINGE .